KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA

CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI

SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 2, 2020

MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na Mark Finley ni msaidizi wa Mwenyekiti wa Konferensi Kuu.
Mtafsiri: Mch. Herbert I. Nziku – Mratibu - Huduma za Maombi: STUM

Juma la Kwanza: Machi 27 – Aprili 2, 2020

“Amani Katikati ya Janga”

Tarakimu zinazidi kuongezeka. Janga katili la Corona au COVID-19, linasafiri kwa mwendo kasi wa mwanga kulizunguka tufe la dunia. Lakini liko pigo lingine ambalo linakimbia zaidi. Limewaathiri watu zaidi ya coronavirus ilivyowaathiri. Kama ilivyo hatari coronavirus, pigo hilo ni hatari, lakini kuna kitu kingine zaidi ambacho ni cha kufisha – hofu. Hofu na wasi wasi vinaathiri mfumo wetu wa kinga za mwili, vinakatisha furaha yetu, na kupokonya tumaini letu.

Luka 21:26-28
“Watu wakivunjika mioyo kwa hofu, na kwa kutazamia mambo yatakayoupata ulimwengu. Kwa kuwa nguvu za mbinguni zitatikisika. 27 Hapo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika wingu pamoja na nguvu na utukufu mwingi. 28 Basi mambo hayo yaanzapo kutokea, changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia.”

Tuwe tumemezwa na hofu au tumejazwa na tumaini yote yanategemea ni wapi tunakotazama. Kama unayatazama majanga ya asili; kama umemezwa na habari mbaya; kama tauni na magonjwa yamejaza mawazo yako; kama huko ndiko ulikolenga, moyo wako utajazwa na hofu. Yesu anasema, **“Tazama juu!”** Kwa nini? Tunapotazama Patakatifu pa Mbinguni, tunamwona Yesu na kugundua uwezo katika ahadi zake.

Katika kristo tunapata ujasiri. Katika Kristo tunapata uhakikisho. Katika Kristo tunainuliwa juu zaidi ya mashaka ya maisha na wasiwasi na mioyo yetu inajazwa usalama katika yule anayetupenda kwa upendo wa milele, usiokufa, usio weza kuelezewa, usiochoka, na usio na mwisho. Katika Kristo tunakombolewa kutoka kwenye hofu inayotulemaza. Wakati fulani tunaweza kupitia hisia ya hofu, lakini hofu haitatufanya tulegee kwa sababu tumaini letu kwa Mungu linashinda dhidi ya hofu.

Hapa ipo kauli nyingine ya kutia moyo kutoka *Signs of the Times,* Oktoba 9, 1901. Ni maoni kuhusu kauli ya Yesu iliyo kwenye Luka 21. “Mioyo wa wanadamu inawafanya washindwe kwa kuogopa mambo yanayoujia ulimwengu. Lakini wale wanaomwamini Mungu wataisikia sauti yake katikati ya tufani, ikisema**, “Ni Mimi; Msiogope.”**

Hapa kuna kauli ya ajabu ya ziada kutoka katika kitabu cha *Evangelism, Uk.* 65:
“Katika kazi kuu ya mwisho tutakabiliana na mashaka ambayo hatujui namna ya kuyashughulikia, lakini hebu tusisahau kwamba zile nguvu kuu tatu za mbinguni zinatenda kazi, kwamba mkono wa Mungu upo kwenye gurudumu, na kwamba Mungu atayatimiza makusudi yake”

Biblia inasema, **“usiogope”** kwa kurudia rudia. Ingawa mimi binafsi sijahesabu ni mara ngapi Biblia imetumia maelezo ya “usiogope,” mwandishi mmoja amehesabu na kupata kwamba yametumika mara 365 katika Biblia nzima – ikimaanisha neno moja katika kila siku kwa mwaka mzima. Mungu amefanyia kazi kalenda ya mwaka mzima. Anatualika tupumzike katika amani yake, tuitumainie neema yake, na kufurahia uweza wake.

Katika moja ya ahadi za Biblia yenye uhakikisho zaidi, Isaya anatutia moyo, akitoa mwangwi wa maneno ya Bwana wetu: **“usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu.” (Isaya 41:10).** Imani yetu inashiukilia ahadi za Neno la Mungu. Nuru yetu inang’aa kwenye giza la ulimwengu huu. Janga la sasa la COVID-19 linaweza kuwa ni kichocheo cha kutuongoza kwenye uhusiano wa kina na Mungu, amani kubwa zaidi, na uzoefu wa maombi ya kina. Katika nyakati za zahama imani yetu iko katika yeye. Tumaini letu liko katika yeye. Yeye ndio usalama wetu, uwezo wetu na tumaini letu. Hebu hili janga linaloendelea liwe ni wito wazi kwa ajili ya toba, uamsho, na matengenezo. Hebu uwe ni wakati ambao tunaishikilia ahadi yake kwamba kesho iliyo bora inakuja!

Maswali ya Moyoni
Katikati ya ulimwengu uliojazwa vurugu, ni wapi tunakoweza kupata usalama wetu na ni wapi tunakoweka imani yetu? Je! Ni katika sayansi au katika kile wanachosema wataalamu wa tiba? Ni katika usalama unaotokana na kazi zetu au katika uhusiano wetu, au ni katika Yesu na ahadi za Neno la Mungu? Ikiwa kweli Yesu ndiye msingi wa imani yetu, ni kwa namna gani umuhimu na lengo la maombi yetu ya kila siku vinabadilika wakati wa hili janga tunalikabiliana nalo?

Changamoto Hai ya Moyo

Kabla Yesu hajarudi, inatupasa kuwa na utegemezi wetu wote na tumaini katika yeye. Hebu tuanze kuomba leo ili kwamba atupatie amani, aimarishe imani yetu katika Neno lake, na atujaze Roho Mtakatifu ili tuweze kumfanyia kazi kwa mafanikio, hata katikati ya janga hili. Hebu tuanze kudai ahadi za 2 Nyak. 7:14, Luka 11:13, na Zekaria 10:1 tunapoomba kila siku kwa ajili ya ujazo wa kina wa Roho Mtakatifu na kwa uponyaji wa nchi yetu.

GC, uk. 621

Kipindi cha dhiki na uchungu kilicho mbele yetu kinahitaji imani inayoweza kuhimili uchovu, kuchelewa, na njaa – imani ambayo haitazimia hata kama itajaribiwa vikali. Muda wa matazamio umetolewa kwa wote ili kujiandaa kwa ajili ya wakati huo. Yakobo alishinda kwa sababu alikuwa mvumilivu na aliamua. Ushindi wake ni ushuhuda wa maombi yasiyokoma. Wote watakaoshikilia ahadi za Mungu, kama alivyofanya, na kuwa na bidii na wavumilivu kama alivyokuwa, watafanikiwa, kama alivyofanikiwa. Wale ambao hawataki kukataa ubinafsi, kuugua mbele za Mungu, kuomba kwa muda mrefu na kwa dhati kwa ajili ya baraka zake, hawatazipokea. Kupambana na Mungu – ni wachache sana wanaojua maana yake ni nini! Ni wachache sana ambao roho zao zimewahi kuvutwa kumfuata Mungu kwa shauku kubwa hadi kila nguvu inapokuwa chini. Wakati mawimbi ya kukata tamaa ambayo hakuna lugha inayoweza kuyaelezea, yanapomkumba mwombaji, ni watu wachache wanaoshikilia ahadi za Mungu kwa imani isiyoyumba."

Mapendekezo ya aya za ziada za kusoma juma hili

- EGW, "The Last Crisis" 9T11-18
- Mark Finley, Revive Us Again (Tuamshe tena)

SIKU YA 1 - MAMBO YA KUOMBEA

Ijumaa, Machi 27, 2020

1. Omba kwa ajili ya kanisa la Mungu ili lisimame imara katikati ya zahama ya kiafya ya COVID-19 inayoukabili ulimwengu. Tuwaombee wataalamu wetu wengi wa afya, madaktari, wauguzi na wengine wanaofanya kazi kwa saa nyingi kuokoa maisha.

2. Ombea washiriki wetu wa kanisa hasa katika nchi za Italia, Ufaransa, Hispania, Ujerumani, kwani hayo ni maeneo yanayoshambuliwa zaidi na janga la COVID-19 kule Ulaya.

3. Tuwaombee washiriki na watendakazi wa afya katika jiji la New York, ambalo ni eneo lilnaloshambuliwa zaidi katika nchi ya Marekani

4. Tuombe kwamba janga la coronavirus lisiendelee kusambaa, na kwambu Mungu asikie kilio cha watu wake na kuiponya nchi yetu

5. Tuombe kwamba katikati ya machafuko, Wakristo wa ulimwengu wote wahisi ukaribu wa Yesu kurudi na kushinikiza kiti cha mbinguni kwa njia ya maombi kwa ajili ya Roho Mtakatifu.

SIKU YA 2 - MAMBO YA KUOMBEA

Jumamosi, Machi 28, 2020

Yohana 14:27
"Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga."

"Adui hawezi kumchukua kutoka mkononi mwa Mkristo yule ambaye anatumainia tu ahadi zake (Mungu)"

1. Omba kwamba badala ya hofu iwepo amani, na kwamba sisi kama watu tuweze kusimama imara katikati ya machafuko, tukitumaini kwamba Mungu ndia anayedhibiti mambo.

2. Tuwaombee wale wanaohangaika na coronavirus na wale waliowapoteza wapendwa wa katika janga hili. Omba kwa ajili ya tumaini na faraja katikati ya maumivu.

3. Tuwaombee washiriki nchini Kenya, na nchi zingine za Afrika kwa sababu masoko yao ya sehemu za wazi yanafungwa.

4. Tuwaombee Wainjilisti wa Vitabu, wahubiri, walimu wa Biblia, na wengine ambao huenda hawataweza kuendelea na huduma za uso kwa uso kama ilivyokuwa hapo kabla. Omba kwa ajili ya hekima ya Mungu na mawazo mapya ili kupata njia mpya za kutoa huduma.

5. Tuyaombee makanisa ambayo yamefungwa kwa ajili ya coronavius. Tuombe kwamba makusanyiko yabuni njia za kuwa "pamoja" kwa njia ya mtandao na kushuhudia kwa njia zinazofaa, bila kuhatarisha afya zao.

SIKU YA 3 - MAMBO YA KUOMBEA

Jumapili, Machi 29, 2020

Zaburi 139:23, 24
“Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu, Unijaribu, uyajue mawazo yangu; 24 Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, Ukaniongoze katika njia ya milele.”

1 SM, uk. 124
“Hakuna kitu anachokiogopa zaidi Shetani kama kwa watu wa Mungu kusafisha njia kwa kuondoa vikwazo, ili kwamba Bwana aweze kumwaga Roho wake juu ya kanisa linalodhoofika... Kila jaribu, kila mvuto wa upinzani, uwe wa wazi au wa siri, unaweza kupingwa ka mafanikio, “Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi.” (Zekaria 4:6)

1. Omba kwamba tulichukue ombi la Daudi katika Zaburi 139 kuwa la mtu binafsi, tukimwomba Bwana kwamba ikiwa kuna kitu cho chote kinachosimama kati yetu na yeye, kama Roho Mtakatifu atafunua jambo fulani, tuweze kuungama na kuyaweka mambo sawa na Mungu na wengine.

2. Tuombe kwamba tuweze kuishi kwa imani, sio kwa hofu, bila kujali mazingira yanayotuzunguka.

3. Tuombe kwa ajili ya mahitaji ya wale wanaopoteza kazi, wanaoachishwa kazi, au wale wasio na uhakika wa mlo unaofuata kama wasipoenda kazini. Tuombe kwamba Mungu awategemeze na kuwapatia mahitaji yao ya kila siku kama aliyoahidi kuwa atafanya katika Isaya 33:6 na Wafilipi 4:19

4. Omba kwamba washiriki wa kanisa ulimwenguni kote waelewe kwamba Kanisa la Waadventista wa Sabato ni vuguvugu la kiunabii likiwa na ujumbe wa kiunabii lilioaminiwa na Mungu likiwa na utume maalum sana wa kiunabii, na sasa ndio muda wa kuangaza kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

5. Tuombe kwamba viongozi wote wa kanisa na washiriki mahali kote waweze kuona kwamba hili pumziko lisilo na mikutano na ajenda liwe kama fursa ya kukuza matembezi ya kina pamoja na Yesu.

SIKU YA 4 - MAMBO YA KUOMBEA

Jumatatu, Machi 30, 2020

Zaburi 91:6-7
“Wala tauni ipitayo gizani, Wala uele uharibuo adhuhuri, 7 Ijapo watu elfu waanguka ubavuni pako. Naam, kumi elfu mkono wako wa kuume! Hata hivyo hautakukaribia wewe.”

3 T 555
Imani huwa imara kwa kukabiliana na mashaka na mivuto ya upinzani. Uzoefu unaopatikana katika majaribio hayo ni yenye thamani kuliko vito vya thamavi.”

1. Tumwombe Mungu atimize ahadi ya Zaburi 91 na awazungushie wigo watoto wake, akiwalinda dhidi ya pigo la coronavirus linalougubika ulimwengu.

2. Tuombe kwamba janga hili liwe ni hatua ya mgeuko katika historia ya kanisa, na kwamba watu wafumbuliwe macho yao ili waone namna Yesu, alivyo karibu kuja.

3. Tuwaombee wale wanaoishi kwenye nyumba zenye msongamano kwenye majiji makubwa, ili wapate njia za kiubunifu za kuwafanya wadumu kuwa wenye afya na kujiunganisha na wengine. Tuwaombee kwa namna ya pekee watoto waliofungiwa ndani.

4. Tuombe hekima kwa ajili ya uamuzi mwingi unaoukabili uongozi wa kanisa la ulimwengu kwa sasa. Tuombe hekima ya Mungu kwa ajili ya wakati huu wenye changamoto.

5. Tuome hekima kwa ajili ya serikali zetu na viongozi wa ulimwengu wakati huu mgumu. Tuombe kwamba kuwepo na kumtafuta Mungu miongoni mwa viongozi wa ngazi za juu na maofisa wa serikali.

SIKU YA 5 - MAMBO YA KUOMBEA

Jumanne, Machi 31, 2020

Luka 11:13
“Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?”

RH, March 19, 1895
“Kushuka kwa Roho Mtakatifu juu ya kanisa kunaonekana kama ni jambo la wakati ujao; lakini ni fursa ya kanisa kupoea sasa. Tutafute sasa, tuombe sasa, na tuamini. Ni lazima tupokee, na mbingu zinasubiri kumtoa.”

1. Omba kwa ajili ya wale wenye maambukizi mapya ya COVID-19. Omba Mungu atupatie hekima na njia za matibabu.

2. Tuombe kwamba washiriki wa kanisa la Waadventista wa Sabato wawe mstari wa mbele katika kuweka kielelezo cha mtindo wa maisha ya kiafya na njia za asili za kuimarisha mfumo wa kinga za mwili, kama vile kula matunda mengi na mboga za majani, kuoga maji ya moto na ya baridi (kwa kupokezana), na kufungua madirisha ili kupata hewa safi.

3. Tuombeane kama kanisa ili tujue namna inayofaa ya kuutumia na kuwaelekeza wengine ujumbe wa afya kama, **“mkono wa kuume wa injili”** kwa kutoa elimu kwa njia ya mtandao, video na njia zingine za kiubunifu.

4. Tuome kwamba badala ya kuutumia muda wa kuwepo majumbani kwa kupata maburudisho ya kidunia, tuweze kuutumia kujifunza Neno la Mungu, kuomba na kusoma vitabu na kutazama video zitakazo kuza imani yetu.

5. Tuyaombee makanisa ulimwenguni kote yatengeneze mipango ya namna ya kuwafanya washiriki wadumu katika mwunganiko wakati huu tuliotenganishwa kwa sababu ya hili janga.

SIKU YA 6 - MAMBO YA KUOMBEA

Jumatano, Aprili 01, 2020

Zaburi 55:16 – 18
Nami nitamwita Mungu, Na Bwana ataniokoa; 17 Jioni, asubuhi, na adhuhuri nitalalama na kuugua, Naye ataisikia sauti yangu. 18 Ameiokoa nafsi yangu iwe salama, asinikaribie mtu, Maana walioshindana nami walikuwa wengi.

1 SM 116
"Kanisa litakapoamka katika ufahamu wa wito wake mtakatifu, maombi mengi ya bidii na nguvu yatapanda mbinguni kwa ajilia ya Roho Mtakatifu ili atuoneshe kazi na jukumu la watu wa Mungu kuhusiana na wokovu wa roho.Tunayo ahadi ikitungoja kwamba Mungu atasogea karibu kwa kila roho yenye kutafuta"

1. Tuombe kwa ajili ya Babu na Bibi zetu, wazazi wetu, na wazee ili wawe na nguvu na afya katikati ya hii zahama ya ulimwengu mzima.

2. Tuwaombee wataalamu wetu wa afya, madaktari na wauguzi, na wengine wanaoendelea kufanya kazi saa zote katika kuhudumia wagonjwa wa Coronavirus wanaozidi kuongezeka. Tuwaombee wawe na afya njema na usalama.

3. Tuombe kwamba Ujumbe wa Malaika Watatu usonge mbele, tena kwa nguvu zaidi katika maeneo ya ulimwengu ambako matukio makubwa ya uinjilisti yalikuwa yamepangwa kufanyika na sasa yameahirishwa, macho yote yaelekezwe mbinguni.

4. Tuombee mikakati ya Injili Katika Majiji kwenye maeneo mbalimbali ya Kanisa la Ulimwengu. Tuombe kwamba mbegu zilizopandwa tayari wakati huu ziweze kuzaa matunda kwa ajili ya ufalme wa Mungu.

5. Tuombe kwa ajili ya hekima, uvumilivu na neema katika kushughulika na mabadiliko mengi yanayotokea katika maisha ya kila siku, ili watu waweze kuchukuliana nayo, na zaidi ya hayo wawe mashahidi waaminifu kwa uongozi wa Mungu wenye nguvu katika maisha yao.

SIKU YA 7 - MAMBO YA KUOMBEA

Alhamisi, Aprili 02, 2020

Zaburi 50:15
"Ukaniite siku ya mateso; Nitakuokoa, na wewe utanitukuza."

PP, 203
"Yakobo alishinda kwa sababu alikuwa mvumilivu na aliyeamua. Uzoefu wake ni ushuhuda wa nguvu ya maombi yasiyokoma. Ni sasa tunapotakiwa kujifunza somo hili la maombi ya ushindi, ya imani isiyoyumba. Ushindi mkubwa kwa kanisa la Kristo au kwa Mkristo binafsi sio ule unaopatikana kwa njia ya talanta au elimu, kwa utajiri au kwa mapenzi ya watu. Ni ushindi ule unaopatikana kwenye chumba cha Mungu cha kusikilizia maombi, wakati imani ya dhati na yenye uchungu inapoushukilia mkono wenye nguvu wa uweza."

1. Tuombe kwamba tuendelee kumtazama Mungu kwa imani, tukimtumainia katika mashaka yetu ya wakati ujao, tukijua kuwa yenye ndiye anayedhibiti mambo yote. Tuombe kwamba tuwe na uwezo wa kulitumainia Neno la Mungu hata wakati hali inayotuzunguka inapoonekana kuwa ni ya giza na yenye kukatisha tamaa.

2. Tuwaombee viongozi na watawala wa kanisa wapate hekima wanapoendelea kufanyia kazi changamoto za mabadiliko ya maandalizi ya Sesheni ya Konferensi Kuu, ambayo sasa itafanyika Mei 20 – 25, 2021 kule Indianapolis.

3. Tuombee Sesheni ya Konferensi Kuu ya mwaka 2021 ili ijazwe na mipango ya kiroho na inayolenga mipango ya utume na kwamba Roho Mtakatifu awe na udhibiti kamili.

4. Tuombee mada ya Sesheni ya Konferensi Kuu ya 2021 ambayo ni: **"Yesu Anakuja! Shiriki!"** Tuombe kwamba washiriki wote ulimwenguni wauchukulie wito wa TMI kuwa ni wa kila mmoja binafsi.

5. Tuombee Roho Mtakatifu amwagwe kwa wingi kwa washiriki wa kanisa la Mungu katika ulimwengu wote, po pote walipo, ili kazi imalizike na tuweze kwenda nyumbani